WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI
SHIRIKA LA UVUVI TANZANIA (TAFICO)

# MAFANIKIO YA SHIRIKA
## MWAKA WA FEDHA 2024/25

## 1 UNUNUZI WA MELI YA UVUVI WA BAHARI KUU KUPITIA PROGRAMU YA ESDP/JAPAN

Shirika kupitia Programu ya ESDP/JAPAN linaendelea na ujenzi wa Meli moja ya Uvuvi, ambayo ujenzi wake umefikia 65% ikitarajiwa kukamilika Mwezi Novemba, 2025 na kuwasili nchini Mwezi Disemba 2025. Kukamilika kwa ununuzi na kuwasili kwa Meli hii kutaliwezesha Shirika kuanza rasmi Uvuvi wa Bahari Kuu na biashara ya samaki ndani na nje ya nchi. Kiasi cha TZS 5.9 Bilioni zitatumika kukamilisha kazi hizi.




## 2 MAGARI YA UBARIDI (REFRIDGERATED VEHICLES)

Shirika limefanikiwa kununua magari manne (4) kwa ajili ya kusafirishia mazao ya Uvuvi ambayo yana uwezo wa kubeba tani 35 kwa wakati mmoja. Magari haya yamenunuliwa kupitia Program ya AFDP TZS 428,000,000 Milioni na fedha za maendeleo za ndani TZS 481,440,000 Milioni Magari haya ni miongoni mwa miundombinu muhimu katika kufanikisha Uvuvi wa Bahari Kuu na kuimarisha mnyororo wa thamani kwa mazao ya uvuvi.



## 3 UKARABATI GATI YA KUSHUSHIA MELI



Kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II), Shirika linaendelea na ukarabati wa gati ya kushushia meli (Floating jetty) itakayotumika na meli za Shirika, Makao Makuu Ras Mkwavi,Kigamboni jijini Dar es Salaam.

## 4 MTAMBO WA KUZALISHA BARAFU ZA TOFALI

Kwa Mwaka 2024/25 Shirika limefanikiwa kuanza uzalishaji wa barafu za tofali. Kupitia uzalishaji wa barafu Shirika linachangia katika uimarishaji wa mnyororo wa thamani kwa mazao ya uvuvi kwa kupunguza kupunguza upotevu wa Mazao ya Uvuvi. Mtambo huo una uwezo wa kuzalisha tani 5 kwa siku una chumba cha ubaridi chenye uwezo wa kuhifadhi tani sita za barafu. Mtambo huu umegharimu TZS 112,500,000 Milioni.

